

Jinsi Tunavyofanya Kazi

Programu ya Viongozi Chipukizi kwa Ajili ya Mabadiliko

Watetezi vijana ndio nguvu ya kuelekea mustakabali wenye usawa zaidi. Vijana tayari wanabadilisha ulimwengu, wanaleta mitazamo yao ya kipekee, utaalamu, na uzoefu wao wenyewe ili kuleta athari katika jamii zao, nchini na kimataifa. Kama wadau katika siku zijazo za sayari yetu, vijana wanastahili kushika usukani kuhusu sera na programu zinazowaathiri, zinazoathiri jamii zao na ulimwengu.

Kwa zaidi ya miaka 10 , Shirika la Women Deliver limeunga mkono utetezi wao kwa kutoa zana na nyenzo kwa viongozi vijana ili kutetea mabadiliko muhimu wanayotaka kuona kuhusiana na afya na haki za ujinsia na uzazi (SRHR).

Tunalenga kubadilisha mamlaka yawe mikononi mwa wale walio karibu na wamepitia changamoto zinazowakabili wasichana.

Programu yetu ya Viongozi Chipukizi kwa Ajili ya Mabadiliko ni programu yetu mpya ambayo imepata msingi wake kutokana na ushirikiano wetu wa zaidi ya miaka 10 na vijana viongozi watetezi. Programu hii inatokana na imani kwamba kuwekeza kwa Viongozi Chipukizi ambao wako karibu zaidi na jamii zao na mahitaji ya wasichana waliobalehe, ni muhimu katika kuhakikisha kuwa suluhisho kwa changamoto zinazokumba SRHR, changamoto wanazokabiliana nazo wasichana waliobalehe, ni suluhisho zinazowalenga vijana na kushughulikia kwa njia ya kipekee mahitaji na changamoto za mazingira yao husika. Programu hii pia imeundwa kutokana na uzoefu wetu wa miaka 10 wa kufanya kazi na watetezi wa vijana, hasa kupitia Programu ya Vijana Viongozi.



Je, Viongozi Chipukizi ni kina nani?

Viongozi Chipukizi ni watetezi wa SRHR (wenye umri wa miaka 15-29) walio katika hatua za mwanzo za safari yao ya utetezi. Programu hii inaunda vuguvugu kubwa la Viongozi Chipukizi, Viongozi Vijana Waliohitimu, na watetezi wa vijana ambao wanaweza kuendeleza na kuimarisha mapambano ya uhuru wa kimwili. Wakifanya kazi katika ngazi ya kitaifa, kikanda, na kimataifa, viongozi hawa vijana watawajibisha serikali zao ili kutoa SRHR katika mipango ya huduma ya afya kwa wote (UHC), kuhakikisha mtazamo wenye haki wa kuzingatia jinsia katika hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kulinda SRHR.

Viongozi Chipukizi - ingawa kwa bahati mbaya mara nyingi hupuuzwa na watoa maamuzi walio mamlakani - wana ujuzi na uzoefu wa maisha ambao ni muhimu ili kufikia uhuru wa kimwili wa wasichana waliobalehe. Programu hii inalenga kuleta sauti na suluhu zao kwa kujenga wasifu wao ili watambuliwe kama wataalam na viongozi katika SRHR na waweze kufikia majukumu na nafasi za kufanya maamuzi.

Je, ni kwa Njia Gani?

Shirika la Women Deliver litawekeza katika Viongozi Chipukizi kupitia utoaji wa ruzuku, hatua za pamoja, ushiriki wa kisiasa, kujifunza na kubadilishana maarifa, usaidizi wa kiufundi, ufikiaji wa nafasi za kimataifa, na fursa za kuzungumza, ufikiaji wa vyombo vya habari na uongozi. Pia tuna rekodi iliyothibitishwa ya kutetea uongozi wa vijana na ushirikiano wenye usawa katika masuala ya SRHR na haki na usawa katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi, na nafasi za ushawishi. Kwa kupata msingi wake katika mwongo mmoja wa kufanya kazi na watetezi vijana kupitia Programu ya Vijana Viongozi , tunaunga mkono harakati za kifeministi, wanaharakati, na watetezi wanaofanya kazi kulinda na kuendeleza afya na haki za wasichana waliobalehe na kuunda mfumo mzuri wa mashirika ya watetezi ambayo yataendelea kutetea na kupigania mabadiliko ya kijamii kwa miaka mingi ijayo.

Jinsi Tunavyofanya Kazi

Tunaendeleza afya na haki za wasichana waliobalehe kwa kuunda nafasi kwa ajili ya hatua za pamoja, kutetea na kuunga mkono utetezi wa vijana, na kuwaunganisha kukutana na mashirika yenye nia kama hiyo. Katika kila jambo tunalolifanya,



tunalenga kubadilisha mamlaka yawe mikononi mwa wale waliopitia changamoto zinazowakabili wasichana.